Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Sifa Za Kiuhalisiaajabu Katika Riwaya Nne Teule Za Watoto

**Ruth Wangari Mwai[1]; Dr. Ntiba Onesmus Gitonga[2]**
[2] ontiba@yahoo.com
**Main author email:** wangariruth6@gmail.com

## IKISIRI

Utafiti huu unakusudia kutathmini sifa za kiuhalisiaajabu katika riwaya nne teule za watoto ambazo ni: *Mama wa Kambo* (2005) ya Catherine Kisovi, *Karamu Mbinguni* (2002) ya Njiru Kimunyi, *Mkasa wa Fumo Liyongo* (2001) ya Bitugi Matundura na *Chura Mcheza Ngoma* (2001) ya Rebecca. Mtafiti aliteua riwaya nne za watoto kwa kutumia sampuli makusudi. Riwaya hizi ni sehemu ya riwaya hamsini (50) zilizokusanywa zenye data mwafaka na ni baadhi ya miongoni mwa zile ambazo zilipendekezwa na kupitishwa na ile iliyokuwa Taasisi ya Elimu nchini Kenya (K.I.E.) kusomwa na wanafunzi katika darasa la nne hadi la nane na ziliweza kupatikana kwa urahisi kwa madhumuni ya utafiti. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Mtafiti alitumia mbinu ya utafiti ya uchanganuzi wa yaliyomo kama utaratibu wa utafiti wa maandishi. Mtafiti alikusanya data ya kimsingi maktabani. Baadhi ya mihimili yake ndiyo ilitumiwa katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Pia mtafiti alitathmini vitabu husika na kudondoa data iliyohitajika. Jumla ya riwaya nne zilizoandikwa kwa ajili ya watoto zilitumiwa kupata data iliyotakikana katika uchanganuzi. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Hatimaye, data iliyokusanywa ilichanganuliwa. Utafiti huu ulibaini kuwa Kuna matukio ya kiajabu yaliyotumiwa katika riwaya hizi nne za watoto. Aidha sifa za kihalisiaajabu zimebainika wazi katika riwaya hizi. Kwa mujibu wa makala haya ni bayana kwamba uhalisiaajabu umetumika katika riwaya hizi kwa madhumuni ya kuendeleza masuala ibuka kwa hadhira ya watoto.

**Maneno muhimu**: Uhalisiajabu, fasihi ya watoto, fantansia.

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Mwai, R.W. & Gitonga, O. N. (2020). Sifa za kiuhalisiaajabu katika riwaya nne teule za watoto. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 150-162.

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## UTANGULIZI

Waandishi wa fasihi ya watoto hawajaachwa nyuma katika kutumia uhalisiaajabu kama mbinu ambayo inawasilisha ujumbe kwa watoto. Kwa kufanikisha kuiteka saikolojia ya watoto, hulazimu mwandishi wa kazi ya watoto kuiandika kwa njia ya mvuto wa kipekee ili ifurahishe. Mojawapo wa mbinu ya kufanya hivyo ni kutumia uhalisiaajabu. Matumizi ya uhalisiaajabu katika kazi za watoto yamechangia katika kuongezeka kwa wasomaji wa kazi hizi jambo ambalo limefanya fasihi ya watoto iendelee kukua na kupanuka katika tanzu zake na kupata mwamko mpya. Fasihi ya watoto imetambulika kuwa na umuhimu sana katika jamii, hasa ya watoto jambo ambalo linadhihirika kupitia kwenye vyombo vya habari, waandishi wa vitabu, mashirika ya uchapishaji na muhimu kabisa katika mfumo wa elimu.

### MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa mujibu wa katiba ya Kenya kifungu cha 260, mtoto ni mtu wa chini ya miaka kumi na minane kwa sababu hajapevuka kiakili. Vilevile hana idhini ya kuolewa na kuoa na hana uhuru mwingine wa kikatiba kama ule wa kupiga kura. Women Aid Collective (W.A.C) (2002) wakizingatia sheria za watoto wanafasili mtoto kuwa ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minne na mtoto mdogo ni mtu mwenye umri wa miaka kumi na minne lakini ambaye hajatimiza miaka kumi na saba. Katika fasili hii wataalam hawa wanajaribu kuibua tofauti kati ya mtoto na mtoto mchanga. Ufafanuzi huu ni muhimu katika utafiti huu kwa vile riwaya zilizoteuliwa ni za watoto wa umri kati ya tisa hadi kumi na minne.

Uhalisiaajabu ni aina ya uhalisia unaohusisha maajabu; yaani unaelezea uujiza uliomo kwenye uyakinifu wa kila siku. Kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiaajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu. Mbatiah (2001: 60) anafafanua uhalisiaajabu kuwa ni istilahi inayotumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia; yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Wamitila (2003) anaeleza kuwa fantasia ni sawa na njozi. Njozi ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka uhalisia. Anaendelea kufafanua kuwa ni kazi yenye sifa za kindotondoto au kutaka kuamilisha hali isiyo ya kawaida. Njozi hupatikana sana katika maandishi yanayolenga hadhira ya watoto. Fasihi ya watoto ni mojawapo wa kazi ambazo huwa na sifa za kinjozi.

Hivyo basi, uhalisiaajabu kama mbinu katika fasihi ya watoto ina dhima kuu katika uwasilishaji wa ujumbe wake kwani hulenga kuleta mvuto kwa kazi za watoto hali ambayo husaidia katika uelewekaji wa maudhui. Matumizi ya uhalisiaajabu katika kazi za watoto yamechangia katika kuongezeka kwa wasomaji wa kazi hizi jambo ambalo limefanya fasihi ya watoto iendelee kukua na kupanuka katika tanzu zake na kupata mwamko mpya. Fasihi ya watoto imetambulika kuwa na umuhimu sana katika jamii, hasa ya watoto, jambo ambalo linadhihirika kupitia kwenye vyombo vya habari, waandishi wa vitabu, mashirika ya uchapishaji na muhimu kabisa katika mfumo wa elimu. Makala haya yatashughulikia namna sifa za kiuhalisiaajabu zinavyojitokeza katika riwaya nne teule za watoto ambazo ni: *Mama wa Kambo* (2005) ya Catherine Kisovi, *Karamu Mbinguni* (2002) ya Njiru, *Mkasa wa Fumo Liyongo* (2001) ya Bitugi na *Chura Mcheza Ngoma* (2001) ya Rebecca. Sifa za kiuhalisiaajabu zitahakikiwa kwa mujibu wa Zamora (1993), kazi za Danow (1995), Cooper (1998) na Encarta encyclopedia (2002) na ni pamoja na: -matukio yaliyo ya kiajabu ambayo ni ya kushangaza na ya



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kuogofya, kuvunjwa kwa mipaka ya mahali, wahusika na uhusika pamoja na upanuaji wa mwanda wa kisimulizi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisiaajabu. Uhalisiaajabu huelezea uujiza uliomo kwenye uyakinifu wa kila siku. Kwa mujibu wa maelezo ya Zamora na Farris (1995) nadharia ya uhalisiaajabu ilianza mnamo mwaka wa 1925. Mwanzilishi wake alikuwa mhakiki wa sanaa wa Kijerumani aliyeitwa Franz Roh. Dhana ya Roh ya nachexpressionismus, magischer Realismus ikitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili inaashiria hali ya uajabu. Mihimili ya uhalisiaajabu kwa mujibu wa Zamora na Farris (1995), kazi za Danow (1995), Cooper (1998) na Encarta encyclopedia (2002) ni kama ifuatavyo: Mosi, matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Pili, uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiaajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. Tatu, mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, maanake ni kuwa wanauhalisiaajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja. Nne, wakati na mahali zina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Tano, uhalisiaajabu umefungamana na sanaajadi kama vile visasili. Visasili ni hadithi zinazoeleza asili ya watu na matukio fulani. Sita, matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika.

Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Saba, mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Nane, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiaajabu. Tisa, uhalisiaajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbalimbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana. Ni muhimu kutaja kwamba, katika utafiti huu, si mihimili yote ambayo ilitumika. Iliyotumika ni ile tu, iliyofaa zaidi kufafanua riwaya zilizochunguzwa ili kuweza kuangazia dhana ya uhalisiaajabu. Hivyo basi, nadharia hii ya uhalisiaajabu ilisaidia katika ukusanyaji, uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

## MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, sababu za utafiti pamoja na nadharia iliyoongoza utafiti. Baada ya kunakili yaliyomo, data ilipangwa kwa minajili ya kufanyiwa uchanganuzi.Utambuzi wa dhana mbalimbali zilizopatikana katika matini ambazo zinaibua uhalisiaajabu ulifanywa. Sifa za uhalisiaajabu kulingana na mwongozo wa nadharia ya uhalisiaajabu zilifafanuliwa. Baadhi ya sifa zilichanganuliwa kwa sababu ya kutathmini matumizi ya uhalisiaajabu katika riwaya nne teule za watoto na kufafanua umuhimu wake katika riwaya za watoto.

### Matukio ya Ajabu na Kuogofya.

Katika riwaya hizi nne teule za watoto kuna matukio ya kiajabu ambayo yameimbuka kama njia moja ya kuendeleza riwaya hizi. Katika *Karamu Mbinguni* ya Njiru Kimunyi matukio ya kiajabu yamejitokeza kwa wingi. Ndege wanapata mwaliko wa ajabu wa kwenda mbinguni kupitia kwa Mbayuwayu ambaye ni mmoja wa ndege. Mbayuwayu alitoa barua ya mwaliko na la kushangaza ni



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kwamba barua ya mwaliko ilikuwa inameremeta ikipigwa na miale ya jua. Aidha, maandishi hayakuwa ya kawaida bali yalikuwa ya dhahabu na karatasi iliyoandikwa maandishi haya ilikuwa ya fedha.

Uajabu mwingine ni kuhusu vitendo na sifa za ndege hawa. Uelewano na bidii kazini ndio msingi wa mwaliko wao ambao umeandikwa katika vitabu vyote vya dhahabu vya ukumbusho. Aidha mbinguni kwaya za Makerubi na Serafi zilikuwa na magoma ya dhahabu, tarumbeta na gita zenye nyuzi zilizomeremeta. Sauti ya kwaya hizi ilikuwa tamu kuliko milio ya vyombo vya muziki, lango la mbinguni ni la dhahabu tupu na linajifungua. Ndani mna utulivu wa ajabu na malaika pia wana mbawa za dhahabu wenye nyuso za kung'ara kwa furaha. Pia, majina ya waliotenda wema yalikuwa yameandikwa kwa mwaandiko wa dhahabu. Ni kweli kwamba matukio ya aina hii si ya kawaida na ni ya kustaajabisha.

Tukio la Mbayuwayu kufika mbinguni ni la kiajabu. Kwanza kabisa alikuwa amepotea njia, akili zilimruka, nao upepo ukamsukuma juu kwa juu hadi akakosa kujitambua kwa ajili ya hofu ya kupotea. Alisikia kwaya zikiimba sauti tamu sana ambayo hakuwahi isikia. Alipokaribia alipata lango la dhahabu tupu, lango pia lilijifungua, akaingia ndani mlimokuwa na utulivu wa ajabu. Akaona malaika, viumbe waliokuwa na mbawa za dhahabu, nyuso za kung'ara zenye furaha. Haya yote ni maajabu machoni mwa mtoto. Vile vile chakula kilichokuwa kikiandaliwa mbinguni kilikuwa cha ajabu. Kilikuwa kingi. Waliokula chao kutoka kwa maji walichaanganyiwa chakula chao majini, kwenye mito na vidibwi.

Kulikuwa na mito ya maji, maziwa hata asali kwa vinywaji. Pia, waliokula mabuu na wadudu kama vile Kigogota walikuwa wanaandaliwa uwanja mkubwa uliojazwa kwa wadudu watupu. Kujipodoa kwa ndege kulikuwa na uajabu. Ndege walikuwa wamepewa uhuru na uwezo wa kujibadilisha watakavyo na Mungu muumba wao.Wangeomba lolote lingetokea. Kwa hivyo wangejipodoa vizuri sana. Ndege walijipamba upya na mabadiliko ya ajabu yalikuweko kwenye sehemu ya vichwa, midomo, miguu na vidoleni. Kila ndege alijaribu kujifanya maridadi kuliko mwenzake. Bundi alijifanyia mabadiliko ya ajabu kwani hangeweza kuona mchana, macho yake yalipofushwa na miale ya jua. Alitembea kwa kuruka huku na huku bila kuona vizuri aendako. Aliongea kwa sauti na mlio wa kishetani kooni na kinywani mwake. Aidha uso wake aliubadilisha ukawa kama wa mchawi aendaye kuroga na ukafanana na wa pakashume.

Tukio la Kobe kujishikilia kwenye unyoya wa Mbayuwayu kwenda mbinguni ni la kiajabu. Vile vile Mbayuwayu aliwaongoza ndege juu kwa juu bila kutumia dira. Safari ya kwenda mbinguni ilichukua siku saba. Usafi wa uwanja wa mbinguni ulitengenezwa kwa mawe yaliyomeremeta kwa bayana ulistaajabisha. Pia miti ilikuwa tofauti na mingine yote duniani. Ilikuwa na matunda makubwa yaliyoonekana matamu. Viti vilikuwa vya dhahabu na vya vito vingine vilivyozidi dhahabu vililetwa pale uwanjani na malaika. Mbinguni hakuna shida yoyote ndege wakahakikishiwa wakitaka chochote waitishe tu kitajileta kwa mfano upumziko, furaha na mengineyo kama chakula. Adhabu ya Bundi kwa kujibadilisha sura yake ikawa ya kutisha wengine ni tukio la kiajabu. Ilitisha ndege kwani alikuwa amebadilika na kuwa kama mchawi mwenye kutembea usiku. Aliadhibiwa kwamba angeruka usiku na hangeshirikiana na viumbe wengine. Sauti na mlio wake ungekuwa dalili ya mauti kwa hivyo binadamu wangemrushia vizinga vya moto na mawe kila wamwonapo au kumsikia.

Adhabu aliyopewa Mbuni ilikuwa ya kuajabisha. Aliambiwa hataruka kama ndege wengine na angetembea kwa miguu yake miwili maishani mwake



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

yote. Vile vile adhabu aliyopewa Kobe kwa kudanganya eti yeye ni wa jamii ya ndege na kuandamana nao hadi mbinguni ilikuwa ya kumwaacha mtu kinywa wazi. Alipewa nafasi ya kuchagua jinsi ya kuitekeleza adhabu yake. Alichagua njia ya kurudi duniani iliyokuwa ya kustaajabisha. Alisema aruhusiwe aruke kutoka mbinguni hadi duniani. Alimwomba Bundi apashe habari kwa mke wake na jamaa zake kuwa wamtandikie magodoro na blanketi uwanjani pake asije akaumia. Hata hivyo, Bundi hakupasha habari za kweli kwa jamaa ya Kobe. Aliwaambia jamaa wa Kobe kinyume na alivyoambiwa. Aliwaambia kuwa Kobe aliwataka wapange mawe mazito mazito ili aweze kuona nyumba yake vizuri kabla ya kujirusha. Kobe alipojirusha aliangukia mawe kwa mgongo wake. Mawe yakamwingia mwilini, jamaa yake na daktari wakajaribu kuyang'oa lakini wapi! Kobe akasalia kuishi na mawe mgongoni. Matukio haya kwa dhahiri ni ya kustaajabisha na kuogofya sana.

Katika riwaya ya *Mama wa kambo* ya Catherene (2005) ina matukio ya kushangaza. Kitete, mama wa kambo wa Kalaa ana urembo wa kustaajabisha. Urembo wake si wa kawaida. Alikuwa na sauti iliyokuwa kama ya kinanda ambayo ingemtoa nyoka pangoni. Miguu yake ilikuwa ya ajabu na angelijitokeza mbele ya wanawake elfu moja wanaohesabika kuwa warembo wangelijichukia wenyewe kwa jinsi alivyokuwa mrembo kupindukia. Urembo huu unaelezwa ukiwa wa uajabu mno. Mengine yaliyoshangaza ni maajabu yaliyotokea siku moja kutokana na maombi ya Kalaa kwa mwenyezi Mungu asaidiwe na chakula baada ya kunyimwa chakula na mamake wa kambo. Sauti tamu kama ya kinanda aliisikia ikisema:-
"Unapokuwa na njaa imba hivi kila siku"

*Mama nateseka saagalale*
*Sina cha kuliwa saagalale*
*Mama nateseka saagalale*
*Sina cha kuliwa saagalale*

"Utaona meza mbele yako itakayokuwa imeandikwa kwa kila aina ya chakula. Kula ushibe na uiweke kama siri kubwa. Kumbuka binadamu ni hasidi, wakijua watakuharibia. Endelea kuvumilia kwa vile uvumilivu hula mbivu kisha ukimaliza kula, uimbe na meza itaondolewa mara moja"

*Mama nimeshiba saagalale*
*Mama nimeshiba saagalale*

Sauti ilipotoweka Kalaa alijaribu kufanya alivyoambiwa, meza ikashuka ikiwa na vyakula vizuri akala akashiba… uk 35-36 hadi mwili wake ukaanza kuwa na mabadiliko kwa sababu ya shibe, ngozi yake ikang'ara na akaongeza uzito. Aidha kuna maajabu mengine yaliyomfanyikia wakati alitaka kwenda kwenye sherehe. Hakuwa na mavazi mazuri ya kwenda kwenye sherehe hiyo. Hapa ndipo nguo na vitu vyenye uzuri wa ajabu vilimzunguka Kalaa. Alijiona katika mavazi hayo yaliyopendeza na akaweza kwenda kwa sherehe. Baadaye aliporudi kutoka kwenye sherehe nguo nzuri alizokuwa amezivaa zilitoweka akabaki na matambara. Pia pana tukio la kiajabu wakati dadake wa kambo, Pendo anapoolewa na jitu na hata kumezwa nalo. Pendo alifikiria kuwa ameolewa na binadamu aliyekuwa tajiri kupindukia kumbe lilikuwa ni jitu lililokuja kumwangamiza. Anasikika akitoa sauti, "Namezwa!" na mama mpita njia.
Maajabu mengine yalitokea wakati Kalaa alikuwa na majonzi baada ya kuteswa na kudhulumiwa na mama na dadake wa kambo aliposikia sauti kutoka mbali ikimwambia, 'Mwanangu, nyamaza. Usiwe na wasiwasi. Kumbuka katika Biblia Tukufu kuhusu mkono wa Mungu ulioandika ukutani ukiashiria kumalizika kwa ufalme wa Belishaza. Usijali. Mipango ya Kitete haitafanikiwa. Acha kujihurumia.Toka ukajifurahishe kwenye tamasha, lakini jihadhari usifanye urafiki na yeyote. Wageni waliofika si watu wa kawaida. Kumbuka ninayokueleza." … Uk 41. Sauti hiyo ilikuwa ya kuajaabisha na kuogofya.


© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Kuna matukio ya kiajabu katika *Chura Mcheza Ngoma* ya Rebecca Nandwa. Maajabu yanafanyika nyumbani mwa sungura. Wanyama wake wanachoka sana. Walitoa maziwa kidogo na wengine walishindwa kusimama wakati wa kukamuliwa. Kuku nao awali mayai yalikuwa yakijaa ndoo wakati huo yalipatikana mawili au matatu. Jogoo hawakuwika kwa sauti nene kama awali. Sauti yake ilikuwa ya chini na mbaya hivyo hawakuweza kumwamsha Sungura. Wanyama hawakuweza kula chakula chote walichowachiwa. Mbwa walilala kwa uoga na kutowalinda kama ilivyokuwa hapo awali. Nje ya nyumba mlionekana vumbi jingi kana kwamba kulikuwa na watu wengi walishinda wakiruka rukia kule siku nzima. Kumbe Chura ndiye alisababisha uchovu huu wote kwa vile aliwapigia wanyama kigoma na kuwaimbia. Walicheza hadi kuchoka. Wakapumzika halafu wakacheza tena. Tunaambiwa wanyama walijifungulia na kujifunga baada ya kucheza. Kusakata rumba kule kulisababisha unyonge wa wanyama na maziwa kidogo na mayai machache. Wakati mwingine densi ilirudiwa mara tatu hadi wanyama wote wakachoka mpaka wakashindwa kusimama. Mambo haya japo yanaelezwa kama ya kawaida ni ya kuajabisha mno kuona wanyama wakifanya kama binadamu.

Matukio ya kustaajabisha na kuogofya katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo* ya Bitugi yameangaziwa. Liyongo aliwashangaza wengi kwani alikuwa na uwezo wa kucheza ngoma aina ya 'gungu na mwao'….uk 20 ambayo mtu wa kawaida. Ni tukio la kuajabisha pale ambapo Liyongo anamwokoa kijana wa rika lake kutoka kwa mamba mkubwa aliyetokea na kuunasa mguu wa kijana huyo. Kijana alipiga mayowe ya kuhitaji msaada kutoka kwa wenzake. Miongoni mwa kundi la wavulana kumi na watano ni Liyongo tu aliyekuwa na ujasiri wa kupambana na mamba. Wengine walitimua mbio na kutoroka. Liyongo alichukua kigogo na kukipondaponda kichwa cha mamba hadi akauachilia mguu wa yule mvulana huku damu ikimbubujika akatokomea majini.

Mamba hakustahimili pigo hilo hivyo keshoye alipatikana akiwa ameelea katika ufuo wa bahari akiwa amekufa. Kitendo hiki cha Liyongo si cha kawaida na kwa hivyo ni cha kustaajabisha na kuogofya. Vitu alivyovibeba wakati Shida mpenziwe alimsihi waende kuishi miongoni mwa ukoo wake wa Wagalla vilikuwa vingi sana hivi kwamba vingeweza kujaza nyumba. Uajabu ni kwamba mtu wa kawaida hangeweza kuvibeba, lakini Liyongo alikuwa jitu la miraba minne ndio maana aliweza kuvibeba. Alibeba mabegani kana kwamba havikuwa na uzito wa kushtua. Pia alichukua panda tatu za kujiburudisha nazo njiani. Aidha alipokuwa njiani hakujali kuchelewa kufika Pate na alilala kwenye kichaka cha miti kwani alikuwa na uwezo wa kumuua mnyama yeyote. Liyongo alistaajabisha kwa vile alichukua siku mbili tu kutoka Shanga hadi Pate pale ambapo mtu wa kawaida alichukua siku nne. Alipofika Pate alichukua moja ya Panda zake na kupuliza kwa pumzi zote za mapafu yake, ikatoa mlio wa radi na kupasuka vipande vipande. Alichukua ya pili vile vile nayo ikapasuka.

Liyongo aliogofya kwa ushujaa wake kwani tunaambiwa kuwa yeye ni shujaa mnyama asiyelika na fisi. Vile vile ana uwezo wa kukwea mikoma mirefu na kutunda makoma. Alitumia mshale kuyaangusha makoma mengi yaliyokuwa juu ya mkoma mrefu sana kuliko mingine. Makoma aliyoangusha yalikuwa mengi kuliko yaliyochumwa na mashujaa wengine. Kuna uajabu wa kile kingemuua Liyongo Fumo. Alimwambia Moni mwanawe angeuawa kwa kuingizwa msumari wa shaba kwenye sehemu ya kitovu chake ... Uk 84. Aidha ndoto ya Moni ni ya kustaajabisha.

Uk 85….Alitambiwa na nyanyake kuhusu mzee aliyekuwa maskini sana hata hangeweza kukidhi mahitaji ya mwanawe ya kununulia nguo, chakula kizuri au malazi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mema. Hata hivyo alikuwa na kipawa cha utabiri. Uajabu ni kwamba aliweza kutabiri mambo ya siku, miezi na hata miaka ya usoni. Aidha aliweza kuona mipango yote aliyokuwa akipangiwa na wanakijiji wake waliomwonea wivu. Walimweendea ugangani ili wamloge afe. Walipoona hawatafaulu walipanga kumtumia kijana wake kwa kumwahidi zawadi nono kumuua babake. Babake aliweza kuyaona yote. Lingine la kustaajabisha ni ule mkoromo wa Liyongo uliokuwa kama ngurumo za mvua. Pia kifo chake ni cha kustaajabisha kinyume na hali ya kawaida Liyongo alikufa hali amepiga goti moja na kuushika uta wake na mshale uliotayarishwa kufuma. Pia alikaa kwa hali ile kwa siku tatu… Uk 96.

**Kuvunjwa kwa Mipaka ya Mahali**

Matukio katika riwaya za watoto hayajitokezi katika muktadha finyu wa eneo moja. Hali hii hujitokeza ili kutoa ujumbe kwa njia isiyo ya kawaida ili kuvuta makini ya mtoto. Kuna kuvunjwa kwa mipaka ya kimahali katika riwaya ya *Karamu Mbinguni* kwa vile matukio yaliyomo hayajajikita katika mandhari mahsusi. Hii ni kwa sababu ndege wanapata mwaliko wa kwenda mbinguni kupitia kwa Mbayuwayu. Mbayuwayu alileta barua ya mwaliko iliyokuwa na maandishi ambayo hayakuwa ya kawaida bali yalikuwa ya dhahabu na karatasi iliyoandikwa maandishi haya yalikuwa ya fedha kuwalika waende mbinguni kwa vile ndege walikuwa na sifa za uelewano na bidii nyingi kazini.

Tunaambiwa mbinguni, kwaya za Makerubi na Serafi zilikuwa na magoma ya dhahabu, tarumbeta na gita zenye nyuzi zilizomeremeta. Sauti ya kwaya hizi ilikuwa tamu kuliko milio ya vyombo vya muziki, lango la mbinguni ni la dhahabu tupu na linajifungua. Ndani mna utulivu wa ajabu na malaika pia wana mbawa za dhahabu wenye nyuso za kung'ara kwa furaha. Pia, majina ya waliotenda wema yalikuwa yameandikwa kwa mwaandiko wa dhahabu. Vile vile chakula kilichokuwa kikiandaliwa mbinguni kilikuwa cha ajabu. Kilikuwa kingi. Waliokula chao kutoka kwa maji walichaanganyiwa chakula chao majini, kwenye mito na vidibwi. Kulikuwa na mito ya maji, maziwa hata asali kwa vinywaji. Pia, waliokula mabuu na wadudu kama vile Kigogota walikuwa wanaandaliwa uwanja mkubwa uliojazwa kwa wadudu watupu.

Matukio ambayo yametajwa yanaonyesha kuvunjwa kwa mipaka ya mahali kwa sababu matukio haya hayajajikita katika mandhari mahsusi. Kwa mfano, mwaliko wa ndege unafanyika mbinguni nao wanaishi duniani. Mungu ndiye anawaamuru malaika kuwakaribisha mbinguni wanawaletea viti vilivyokuwa vya dhahabu na vya vito vingine vilivyozidi dhahabu pale uwanjani na malaika. Tunaelezwa kuwa ndege wanahakikishiwa mbinguni hakuna shida yoyote wakitaka chochote waitishe tu kitajileta kwa mfano upumziko, furaha na mengineyo kama chakula. Malaika Maserufi na Makerubi wanaimba nyimbo za tumbuizo kwa ndege. Kwa hivyo, mpaka haupo kati ya mbinguni na duniani, kwa sababu shughuli zinazofanyika mbinguni baadaye zinafanyika duniani. Kwa hivyo mpaka wa mahali haupo katika riwaya za watoto.

Kuvunjwa kwa mpaka wa mahali ni pale barua ya mwaliko inatumwa kutoka mbinguni hadi duniani. Ndipo mpaka uwepo, inastahili ndege kuwa na mwaliko mahali fulani duniani lakini mwaliko wa ndege kwenda mbinguni ni tukio ambalo linajitokeza katika hali ya kuuvunja mpaka wa mahali unaojitokeza baada ya sifa za uelewano na bidii kwa ndege. Katika riwaya ya *Mama wa Kambo* kuna kuvunjwa kwa mipaka wakati Pendo anapoolewa na jitu na hata kumezwa nalo. Kwa kawaida binadamu anastahili kuolewa na binadamu mwenzake lakini si jitu bayana ni kwamba mpaka unavunjwa na Pendo anaolewa na jitu. Tunaambiwa kuwa baadaye jitu lilikuja kumwangamiza.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Pendo anasikika akitoa sauti, "Namezwa!" na mama mpita njia.

**Matukio ya Kifantasia**

Katika riwaya hizi za watoto, matukio mengi yaliyozungumziwa ni ya kifantasia kwa sababu katika *Karamu Mbinguni* ya Njiru Kimunyi kuna matukio ya kifantasia, ni jambo la kifantasia ndege kupata mwaliko wa kwenda mbinguni. Uajabu wa barua yenyewe ni wa kifantasia tunaambiwa ilimeremeta ikipigwa na miale ya jua. Aidha, maandishi hayakuwa ya kawaida bali yalikuwa ya dhahabu na karatasi iliyoandikwa maandishi haya ilikuwa ya fedha. Pia mbinguni kwaya za Makerubi na Serafi zilikuwa na magoma ya dhahabu, tarumbeta na gita zenye nyuzi zilizomeremeta. Sauti ya kwaya hizi ilikuwa tamu kuliko milio ya vyombo vya muziki, lango la mbinguni ni la dhahabu tupu na linajifungua. Ndani mna utulivu wa ajabu na malaika pia wana mbawa za dhahabu wenye nyuso za kung'ara kwa furaha. Pia, majina ya waliotenda wema yalikuwa yameandikwa kwa mwaandiko wa dhahabu. Vile vile chakula kilichokuwa kikiandaliwa mbinguni kilikuwa cha kifantasia. Kilikuwa kingi. Waliokula chao kutoka kwa maji walichanganyiwa chakula chao majini, kwenye mito na vidimbwi. Kulikuwa na mito ya maji, maziwa hata asali kwa vinywaji. Pia, waliokula mabuu na wadudu kama vile Kigogota walikuwa wanaandaliwa uwanja mkubwa uliojazwa kwa wadudu watupu. Aidha kujipodoa kwa ndege kulikuwa kwa kifantasia. Ndege walikuwa wamepewa uhuru na uwezo wa kujibadilisha watakavyo na Mungu muumba wao. Ndege walijipamba upya na mabadiliko ya ajabu yalikuweko kwenye sehemu ya vichwa, midomo, miguu na vidoleni. Kila ndege alijaribu kujifanya maridadi kuliko mwenzake. Bundi alijifanyia mabadiliko ya kifantasia kwani hangeweza kuona mchana, macho yake yalipofushwa na miale ya jua. Alitembea kwa kuruka huku na huku bila kuona vizuri aendako. Aliongea kwa sauti na mlio wa kishetani kooni na kinywani mwake. Aidha uso wake aliubadilisha ukawa kama wa mchawi aendaye kuroga na ukafanana na wa pakashume.

Tukio la Kobe kujishikilia kwenye unyoya wa Mbayuwayu kwenda mbinguni ni la kifantasia. Mbayuwayu aliwaongoza ndege juu kwa juu bila kutumia dira. Safari ya kwenda mbinguni ilichukua siku saba. Usafi wa uwanja wa mbinguni ulitengenezwa kwa mawe yaliyomeremeta na hivyo unakuwa wa kifantasia. Pia miti ilikuwa tofauti na mingine yote duniani. Ilikuwa na matunda makubwa yaliyoonekana matamu. Viti vilikuwa vya dhahabu na vya vito vingine vilivyozidi dhahabu vililetwa pale uwanjani na malaika. Adhabu ya Bundi kwa kujibadilisha sura yake ikawa ya kutisha wengine ni tukio la kifantasia. Ilitisha ndege kwani alikuwa amebadilika na kuwa kama mchawi mwenye kutembea usiku. Aliadhibiwa kwamba angeruka usiku na hangeshirikiana na viumbe wengine. Sauti na mlio wake ungekuwa dalili ya mauti kwa hivyo binadamu wangemrushia vizinga vya moto na mawe kila wamwonapo au kumsikia. Aliambiwa hataruka kama ndege wengine na angetembea kwa miguu yake miwili maishani mwake yote. Vile vile adhabu aliyopewa Kobe kwa kudanganya eti yeye ni wa jamii ya ndege na kuandamana nao hadi mbinguni ilikuwa ya kumwaacha mtu kinywa wazi. Alipewa nafasi ya kuchagua jinsi ya kuitekeleza adhabu yake. Alichagua njia ya kurudi duniani iliyokuwa ya kifantasia. Alisema aruhusiwe aruke kutoka mbinguni hadi duniani. Alimwomba Bundi apashe habari kwa mke wake na jamaa zake kuwa wamtandikie magodoro na blanketi uwanjani pake asije akaumia. Hata hivyo Bundi hakupasha habari za kweli kwa jamaa ya Kobe. Aliwaambia jamaa wa Kobe kinyume na alivyoambiwa. Aliwaambia kuwa Kobe aliwataka wapange mawe mazito mazito ili aweze kuona nyumba yake vizuri kabla ya kujirusha. Kobe alipojirusha aliangukia mawe kwa mgongo wake. Mawe yakamwingia mwilini, jamaa yake na daktari wakajaribu kuyang'oa lakini



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

hawakufaulu. Kobe akasalia kuishi na mawe mgongoni. Matukio haya kwa dhahiri ni ya kifantasia.

Katika riwaya ya *Mama wa kambo* ya Catherene (2005) ina matukio ya kifantasia. Kitete, mamake wa kambo pia ana urembo wa kifantasia. Urembo wake si wa kawaida. Alikuwa na sauti iliyokuwa kama ya kinanda ambayo ingemtoa nyoka pangoni. Miguu yake ilikuwa ya ajabu na angelijitokeza mbele ya wanawake elfu moja wanaohesabika kuwa warembo wangelijichukia wenyewe kwa jinsi alivyokuwa mrembo kupindukia. Wimbo wa Kalaa wa kuitisha chakula ulikuwa wa kifantasia. Aliambiwa, unapokuwa na njaa imba hivi kila siku;*Mama nateseka saagalale*

*Sina cha kuliwa saagalale*
*Mama nateseka saagalale*
*Sina cha kuliwa saagalale*

Angeweza kuona meza mbele yake itakayokuwa imeandikwa kwa kila aina ya chakula. Kula ushibe na aiweke kama siri kubwa na akumbuke binadamu ni hasidi, wakijua watamharibia. Aendelee kuvumilia kwa vile uvumilivu hula mbivu kisha akimaliza kula, uimbe"

*Mama nimeshiba saagalale*
*Mama nimeshiba saagalale*

Na meza ingeondolewa mara moja. Yote haya yalifanyika hadi mwili wake ukaanza kuwa na mabadiliko kwa sababu ya shibe, ngozi yake ikang'ara na akaongeza uzito. Aidha kuna ufantasia mwingine unaodhihirika wakati Kalaa alitaka kwenda kwenye sherehe. Hakuwa na mavazi mazuri ya kwenda kwenye sherehe hiyo. Hapa ndipo nguo na vitu vyenye uzuri wa ajabu vilimzunguka Kalaa. Alijiona katika mavazi hayo yaliyopendeza na akaweza kwenda kwa sherehe. Baadaye aliporudi kutoka kwenye sherehe nguo nzuri alizokuwa amezivaa zilitoweka akabaki na matambara.

Pia pana tukio la kifantasia wakati dadake wa kambo, Pendo anapoolewa na jitu na hata kumezwa nalo. Pendo alifikiria kuwa ameolewa na binadamu aliyekuwa tajiri kupindukia kumbe lilikuwa ni jitu lililokuja kumwangamiza. Anasikika akitoa sauti, "Namezwa!" na mama mpita njia.
Kuna matukio ya kifantasia katika *Chura Mcheza Ngoma* ya Rebecca Nandwa.Tunaambiwa wanyama walijifungulia na kujifunga baada ya kucheza. Kusakata rumba kule kulisababisha unyonge wa wanyama na wakatoa maziwa kidogo na Kuku kutaga mayai machache. Wakati mwingine densi ilirudiwa mara 3 hadi wanyama wote wakachoka mpaka wakashindwa kusimama. Mambo haya japo yanaelezwa kifantasia.

Katika *mkasa wa shujaa liyongo* ya Bitugi matukio ya kifantasia yameangaziwa. Ni tukio la kifantasia pale ambapo Liyongo anamwokoa kijana wa rika lake kutoka kwa mamba. Liyongo na marafikize wakicheza katika ufuo wa bahari, mamba mkubwa alitokea na kuunasa mguu wa kijana huyo. Kijana alipiga mayowe ya kuhitaji msaada kutoka kwa wenzake. Miongoni mwa kundi la wavulana kumi na watano ni Liyongo tu aliyekuwa na ujasiri wa kupambana na mamba. Wengine walitimua mbio na kutoroka. Liyongo alichukua kigogo na kukipondaponda kichwa cha mamba hadi akauachilia mguu wa yule mvulana huku damu ikimbubujika akatokomea majini. Mamba hakustahimili pigo hilo hivyo keshoye alipatikana akiwa ameelea katika ufuo wa bahari akiwa amekufa. Kitendo hiki cha Liyongo si cha kawaida na kwa hivyo ni cha kifantasia.

Vitu alivyovibeba wakati Shida mpenziwe alimsihi waende kuishi miongoni mwa ukoo wake wa Wagalla vilikuwa vingi sana hivi kwamba vingeweza kujaza nyumba. Ufantasia ni kwamba mtu wa kawaida hangeweza kuvibeba, lakini Liyongo alikuwa jitu la miraba minne ndio maana aliweza kuvibeba. Alibeba mabegani kana



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kwamba havikuwa na uzito wa kushtua. Pia alichukua panda tatu za kujiburudisha nazo njiani. Panda zilipulizwa katika ngoma nyingi za kitamaduni za Shanga. Aidha alipokuwa njiani hakujali kuchelewa kufika Pate na alilala kwenye kichaka cha miti kwani alikuwa na uwezo wa kumuua mnyama yeyote. Liyongo alistaajabisha kwa vile alichukua siku mbili tu kutoka Shanga hadi Pate pale ambapo mtu wa kawaida alichukua siku nne. Alipofika Pate alichukua moja ya Panda zake na kupuliza kwa pumzi zote za mapafu yake, ikatoa mlio wa radi na kupasuka vipande vipande. Alichukua ya pili vile vile nayo ikapasuka.

Liyongo aliogofya kwa ushujaa wake kwani tunaambiwa kuwa yeye ni shujaa mnyama asiyelika na fisi. Vile vile ana uwezo wa kukwea mikoma mirefu na kutunda makoma. Alitumia mshale kuyaangusha makoma mengi yaliyokuwa juu ya mkoma mrefu sana kuliko mingine. Makoma aliyoangusha yalikuwa mengi kuliko yaliyochumwa na mashujaa wengine. Kuna ufantasia wa kile kingemuua Liyongo Fumo. Alimwambia Moni mwanawe angeuawa kwa kuingizwa msumari wa shaba kwenye sehemu ya kitovu chake ... Uk 84. Aidha ndoto ya Moni ni ya kifantasia. Katika uk 85… alitambiwa na nyanyake kuhusu mzee aliyekuwa maskini sana hata hangeweza kukidhi mahitaji ya mwanawe ya kumnunulia nguo, chakula kizuri au malazi mema. Hata hivyo alikuwa na kipawa cha utabiri. Ufantasia ni kwamba aliweza kutabiri mambo ya siku, miezi na hata miaka ya usoni. Aidha aliweza kuona mipango yote aliyokuwa akipangiwa na wanakijiji wake waliomwonea wivu. Walimweendea ugangani ili wamloge afe. Walipoona hawatafaulu walipanga kumtumia kijana wake kwa kumwahidi zawadi nono kumuua babake. Babake aliweza kuyaona yote. Mambo haya si ya kawaida ni ya kifantasia tu. Pia kifo chake ni cha kifantasia kinyume na hali ya kawaida Liyongo alitoa mkoromo uliokuwa kama ngurumo za mvua na alikufa hali amepiga goti moja na kuushika uta wake na mshale uliotayarishwa kufuma. Pia alikaa kwa hali ile kwa siku tatu… Uk 96. Haya yote ni ya kufikirika tu na hayana uhalisia wowote.

**Wahusika na Uhusika.**

Wamitila (2002), anafafanua wahusika kama viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile na huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, anasema kuwa wahusika ni 'binadamu' wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambuliwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wamitila (2008), anafafanua dhana ya mhusika kama mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za binadamu. Katika riwaya hizi nne za watoto kuna wahusika wa aina mbili ambao ni binadamu na viumbe ambao si binadamu**.** Riwaya ya *Karamu Mbinguni* ina wahusika ambao si binadamu na ndio wanaosababisha tuichukulie riwaya hii ya watoto kama ya ajabu. Kuna Makerubi na Serafi ambao ni malaika walio na mbawa za dhahabu wenye nyuso za kung'ara kwa furaha na wanaunda kwaya za mbinguni na wanaimba kwa sauti tamu kuliko milio ya vyombo vya muziki. Hawa ndio wanawakaribisha ndege mbinguni na ni wahusika ambao si wa kawaida na kwa hivyo wanaipa riwaya sifa ya kiajabu. Shughuli ambazo hao wahusika wanajihusisha nazo ni shughuli za kiajabu ambazo wahusika wa kawaida hawawezi kuzifanya. Kwa mfano kuyawezesha yasiyowezekana kwa kuwawezesha ndege kuwa na makaribisho makubwa sana na ya kufana sana, kupewa chakula cha uchaguzi wao. Walifanya hivi kwa kumsaidia Mungu kufaanya makaribisho hayo. Vilevile karamu kufanyika mbinguni baada ya malaika kuamriwa na Mungu kuipamba na kuiandaa ili ivutie ndege. Kusababisha karamu ya ndege walio duniani kufanyika mbinguni ni matukio ya kiajabu yanayohusisha wahusika wa kiajabu. Kwa hivyo matukio ya kiajabu na wahusika wa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kiajabu wanasababisha kuwepo kwa sifa ya kiuhalisiaajabu.

Aidha kuna ndege kama Kigogota, Bundi, mbayuwayu na Mbuni. Ndege hawa walijipodoa na wakajibadilisha kwa njia ya ajabu. Mabadiliko yalionekana kwenye sehemu ya vichwa, midomo, miguu na vidoleni. Bundi anajipodoa kwa njia ya kustaajabisha hangeweza kuona mchana, macho yake yalipofushwa na miale ya jua. Alitembea kwa kuruka huku na huku bila kuona vizuri aendako. Aliongea kwa sauti na mlio wa kishetani kooni na kinywani mwake. Aidha uso wake aliubadilisha ukawa kama wa mchawi aendaye kuroga na ukafanana na wa pakashume. Kobe, mhusika mwingine aliyejifanya kama wa jamii ya ndege anachangia tuseme riwaya hii ni ya kiajabu kupitia aliyopewa adhabu na mungu ya kujirusha kutoka mbinguni na kwa hivyo anapojirusha aliangukia mawe kwa mgongo wake. Mawe yakamwingia mwilini, jamaa yake na daktari wakajaribu kuyang'oa lakini hawakufaulu. Kobe akasalia kuishi na mawe mgongoni. Matukio haya kwa dhahiri ni ya sifa za kiuhalisiaajabu. Katika riwaya ya *Mama wa kambo* ya Catherene (2005)ina wahusika binadamu kama Kitete, Kalaa, Konelia, mama Tomi, Taadhima, Pendo.Aidha kuna jitu ambalo linamwoa dadake Kalaa na ndiye anachangia kusema kuwa riwaya hii ina uhalisiaajabu. Kitendo chake cha kumumeza Pendo ni cha kiajabu. Pia Sauti inayozungumzia Kalaa kumweleza jinsi ya kupata chakula na inayomzungumzia kumwambia kuhusu aina ya wageni ambao hawakuwa watu wa kawaida waliokuwa wamefika kwao kutaka posa kwake na hatimaye kunyakuliwa na dadake wa kambo Pendo. Baada ya kuzungumziwa anajiona amezungukwa na nguo na vitu vingi vya uzuri wa ajabu

Kuna wahusika katika *Chura Mcheza Ngoma* ya Rebecca Nandwa ambao si binadamu na ndio wanachangia kusema kuwa riwaya hii ni ya kihalisiaajabu. Wanyama kama Sungura, Chura, watoto wa Sungura, Kuku, ng'ombe walifanya mambo ya kuajaabisha kinyume na jinsi wanyama hufanya. Ng'ombe kwa mfano walijifungulia na kujifunga baada ya kucheza densi. Sungura na watoto wake wanatumia rungu, mapanga na majembe kumshambulia Chura jambo ambalo tunaliona likiwa la kuaajabiwa kwani ni vigumu kwa hali kama hii kuaminika kwa vile linakiuka uhalisia. Katika *mkasa wa shujaa liyongo* ya Bitugi kuna mhusika ambaye si wa kawaida. Liyongo anamwokoa kijana wa rika lake kutoka kwa mamba mkubwa alikuwa na ujasiri wa kupambana na mamba. Aidha vitu alivyovibeba kwenda kwa Wagalla vilikuwa vingi sana hivi kwamba vingeweza kujaza nyumba kwani alikuwa jitu la miraba minne ndio maana aliweza kuvibeba. Alibeba mabegani kana kwamba havikuwa na uzito wa kushtua. Pia alichukua panda tatu za kujiburudisha nazo njiani. Aidha alipokuwa njiani hakujali kuchelewa kufika Pate na alilala kwenye kichaka cha miti kwani alikuwa na uwezo wa kumuua mnyama yeyote. Vile vile Liyongo alistaajabisha kwa vile alichukua siku mbili tu kutoka Shanga hadi Pate pale ambapo mtu wa kawaida alichukua siku nne na alipofika Pate alichukua moja ya Panda zake na kupuliza kwa pumzi zote za mapafu yake, ikatoa mlio wa radi na kupasuka vipande vipande. Alichukua ya pili vile vile nayo ikapasuka. Liyongo Fumo hangeweza kuuawa kama binadamu wengine wa kawaida. Alimwambia Moni mwanawe angeuawa kwa kuingizwa msumari wa shaba kwenye sehemu ya kitovu chake ... (Uk 84). Hii ndiyo maana sababu riwaya hii inakuwa na sifa za kiuhalisiaajabu.

**Upanuaji wa Mwanda wa Kisimulizi**

Wamitila, (2008) anadai kuwa riwaya za aina hii hazina mipaka wazi ya mianda ya kisimulizi na huweza kuhusisha ulimwengu dhanifu au ulimwengu wa njozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti kuvunjwa kiasi kwamba matukio ya ulimwengu wa njozi yanafuata kanuni zile zile za matukio ya ulimwengu halisi. Katika riwaya hizi za watoto sifa ya upanuaji wa mwanda wa kisimulizi ilijitokeza. Sifa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|
Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org
Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

hii imedhihirika katika *Karamu Mbinguni* pale mtunzi wa riwaya hii ameisababisha hali ambapo hakuna mpaka kati ya dunia na mbingu, kwani matukio yanayoijenga riwaya hii yanafanyika katika sehemu hizi mbili. Tunapata maandalizi ya karamu ya ndege yanafanyika duniani. Baada ya maandalizi karamu inakuwa mbinguni. Vilevile adhabu ya wale waliokiuka mapenzi ya mungu inafanywa mbinguni na inakamilikia duniani. Kwa hivyo tunaona kuwa mpaka kati ya mbinguni na duniani umevunjwa kwa sababu matukio yanaingiliana kiasi kwamba msomi anashindwa kueleza iwapo kuna mpaka kati ya mbinguni na duniani, ufinyu umedhihirika kiasi kwamba shughuli zinafanyika kana kwamba ni vijiji viwili vinavyokaribiana. Tunapata kuwa baada ya matendo mema ya ndege Mungu anawapa mwaliko kupitia barua inayopewa Mbayuwayu. Karamu haiwezi fanyika bila maandalizi kabambe ndiyo maana Mungu anawapa uwezo wa kujipodoa kwa jinsi kila mmoja angependa. Aidha Mungu anawaandalia vyakula vya kila nui. Shughuli ya karamu inafanyika Mbinguni utadhani inafanyika duniani. Kwa hakika hakuna mpaka kati ya mbingu na dunia katika matukio tuliyoyataja. Katika *Mama wa Kambo* kuhusu kuoa kwa Baraka mtoto wa mfalme wa ughaibuni tunapata kuwa sifa ya upanuaji wa mwanda wa kisimulizi imedhihirika. Hii ni kwa sababu inasemekana kuwa wakati wake; Baraka ulipofika wa kuoa alitembelea nchi nyingi akitafuta mke na wakati huo wote alivaa kimaskini ili mwanamke yeyote ambaye angekubali kuolewa naye basi angekuwa ni mwanamke halisi … uk. 59. Kijana huyu anatembea nchi nyingi. Kila pembe ya nchi alizunguka akitafuta mwanamke halisi. Kalaa anamkubali akiwa hivyo.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### Hitimisho

Ni dhahiri shahiri kwamba uhalisiaajabu umejitokeza kwa mapana zaidi katika riwaya hizi nne za watoto. Kuna matukio ya kiajabu yaliyotumiwa katika riwaya hizi nne za watoto. Aidha sifa za kihalisiaajabu zimebainika wazi katika riwaya hizi. Kwa mujibu wa makala haya ni bayana kwamba uhalisiaajabu umetumika katika riwaya hizi kwa madhumuni ya kuendeleza masuala ibuka kwa hadhira ya watoto. Masuala ambayo ni ya umuhimu mkubwa kwa maisha ya mtoto. Matumizi ya uhalisiaajabu katika riwaya hizi yanayafanya masuala haya yaeleweke kwa mtoto kwa njia ya kumtia hamasa na shauku ya kusoma na kusoma zaidi riwaya hizi bila kudororeka.

### Mapendekezo

Makala haya yameshughulikia sifa za kiuhalisiaajabu katika riwaya nne teule za watoto. Yametumia riwaya nne za watoto, ningependekeza waandishi wengine washughulikie sifa za kiuhalisiaajabu katika riwaya zingine za watoto. Aidha, wanaweza kutumia tamthilia na hadithi fupi za watoto.

## MAREJELEO

Bitugi, M. (2001). *Mkasa wa Shujaa Liyongo.* Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.

Catherene N. W. K. (2005). *Mama wa Kambo*.Phoenix publishers Ltd. Nairobi.

Cooper, B. (1988). *Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.

Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Literature: Seeing with a ThirEye*. New York: Routledge.

Danow, K. D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque*. Kentucky University of Kentucky Press.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

**Volume: 02 Issue: 01 | Oct-2020|**
**Received: 01.10.2020; Accepted 03.10.2020; Published on 31.10.2020 at www.editoncpublishing.org**
**Mwai, R. W., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

Encarta Encyclopaedia (2002). New York. Microsoft Company Limited.
Fourth Dimensions, Enugu.
Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics & Publishers.
Njiru, K. (2002). *Karamu Mbinguni*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.
Rebecca, N. (2001).*Chura Mcheza Ngoma*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.
Wamitila, K. W (2002). *Uhakiki wa Fasihi; Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi Phoenix Publishers Ltd.
Wamitila, K. W (2008). *Kazi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers. Warnes.
Wamitila, K.W (2003): *Kichocheo cha Fasihi.Nairobi*. Focus Publication ltd.
Women Aid Collective (W.A.C) (2002). *Girls Not brides: The Global partnership to end child marriage.* England and Wales.
Zamora P. L., & Faris B.W. (1995). *Margical Realism: Theory, History and Community*. London. Duke University Press



**© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org**